WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

TANGAZO LA UFADHILI WA MASOMO YA SHAHADA YA UMAHIRI (MASTER'S) KATIKAFANI ZA SAYANSI YA TAKWIMU NA AKILI UNDE (DATA SCIENCE AND ARTIFICIAL INTELLIGENCE) KUPITIA PROGRAMU YA UFADHILI WA SAMIA (SAMIA SCHOLARSHIP EXTENDED-DS/AI+), 2026/2027

A. UTANGULIZI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza Programu maalum ya **SAMIA SCHOLARSHIP EXTENDED DS/AI+** inayolenga kuongeza na kukuza ujuzi wa vijana wa Kitanzania katika fani za Sayansi ya Takwimu, Akili Unde na Sayansi Shirikishi (Data Science, Artificial Intelligence and Allied Sciences) ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira nchini na kuchangia maendeleo ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Wizara inatangaza fursa za ufadhili wa masomo katika ngazi ya Shahada ya Umahiri kwa wahitimu wenye ufaulu wa juu katika fani za Sayansi ya Takwimu (Data Science), Akili Unde (Artificial Intelligence) na fani shirikishi kama vile Ujifunzaji wa Mashine (Machine Learning), Usalama wa Mitandao (Cybersecurity), Sayansi ya Kompyuta (Computer Science), Uhandisi wa Kompyuta (Computer Engineering) na Uhandisi wa Programu za Kompyuta (Software Engineering).

.

B. MAENEO YA UFADHILI

SAMIA SCHOLARSHIP EXTENDED (DS/AI+) itatoa ufadhili wa masomo ya Shahada ya Umahiri utakaogharamia maeneo yafuatayo:

i. Ada ya Mafunzo;

ii. Posho ya Chakula na Malazi;

iii. Posho ya Vitabu na Viandikwa;

iv. Mahitaji Maalumu ya Kitivo;

v. Gharama za Utafiti;

vi. Bima ya Afya.

C. TAASISI INAYOLENGWA

Ufadhili utatolewa kwa waombaji waliopata udahili wa kusoma Shahada ya Umahiri katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) iliyopo Arusha, Tanzania.

D. MUDA WA UFADHILI

Wanafunzi watakaofadhiliwa, watagharimiwa kwa kipindi cha miaka miwili(2) kuanzia Mwaka wa masomo 2026/2027.

E. SIFA ZA WAOMBAJI WA UFADHILI

Mwombaji wa ufadhili huu anapaswa kuwa amehitimu shahada ya kwanza na kuwa na sifa zifuatazo:

i. Awe Mtanzania;

ii. Awe amepata udahili wa kusoma Shahada ya Umahiri katika fani ya Sayansi ya Takwimu na Akili Unde (MSc in Data Science and Artificial Intelligence) katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST);

iii. Awe na umri usiozidi miaka 35;

iv. Awe amesoma tahasusi ya sayansi katika Kidato cha Sita na kuwa na ufaulu wa juu hususani katika somo Kuu la Hisabati (Advanced Mathematics) angalau kwa daraja C;

v. Awe na wastani wa GPA usiopungua 3.8 katika shahada ya kwanza.

F. NYARAKA ZA KUAMBATISHA

i. Barua ya udahili (Admission letter);

ii. Nakala ya kitambulisho cha Taifa(NIDA);

iii. Cheti cha kuzaliwa;

iv. Vyeti vya Shule ya Sekondari;

   a. Cheti cha Kidato cha Nne (Form IV);

   b. Cheti cha Kidato cha Sita (Form VI);

v. Cheti cha Shahada ya Kwanza;

vi. Hati ya Matokeo(Academic Transcript) ya Shahada ya Kwanza;

vii. Wasifu Binafsi wa mwombaji (CV).

G. MASHARTI YA UFADHILI

Mwanafunzi atakayepata ufadhili wa **SAMIA SCHOLARSHIP EXTENDED (DS/AI+)** atatakiwa kuzingatia masharti yafuatayo:

i. Anapaswa kusoma, kuelewa na kusaini Mkataba wa Makubaliano ya Ufadhili wa Masomo kati yake na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;

ii. Anapaswa kuwa na akaunti ya Benki kwa jina lake kwa ajili ya kupokea fedha za ufadhili zikazolipwa moja kwa moja;

iii. Hataruhusiwa kubadilisha programu ya masomo aliyofadhiliwa bila idhini ya maandishi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;

iv. Hataruhusiwa kuahirisha masomo, isipokuwa kwa sababu za kiafya,zitakazothibitishwa na chuo husika;

v. Ikiwa mnufaika ataghairi fursa ya ufadhili kabla ya kuanza masomo, atapaswa kuwasilisha taarifa kwa maandishi kwa:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P. 10,
40479 Dodoma.
Barua pepe: ps@moe.go.tz

H. UTARATIBU WA KUWASILISHA MAOMBI YA UFADHILI

i. Maombi ya ufadhili wa masomo yawasilishwe kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kiunganishi kifuatacho: **temis.moe.go.tz**;

ii. Mwombaji anatakiwa kuweka taarifa zake za mawasiliano, ikiwemo barua pepe na namba ya simu inayopatikana;

iii. Maombi yatakayowasilishwa kwa njia tofauti na iliyopendekezwa au baada ya muda wa mwisho hayatashughulikwa.

I. MUDA WA KUWASILISHA MAOMBI

Maombi ya ufadhili wa masomo yawasilishwe kuanzia tarehe **12** Novemba hadi **27** Desemba**, 2026.**

Imetolewa na:
Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Dodoma.
Tarehe 11 Novemba, 2026